



St. Walburg's Nyangao Referral Hospital
P. O. Box. 1002, Lindi Region - Tanzania, Mobile no. +255656227511
Email address: nyangaohospital@gmail.com Website: <http://www.nyangaohospital.or.tz>

06.05.2026

TANGAZO LA KAZI (URGENT)

Hospital ya Rufaa ya Mt. Walburga Nyangao iliyoko Jimbo Katoliki la Lindi na Halmashauri ya Wilaya ya Mtama-Lindi inatangaza nafasi ya kazi kama ifuatavyo;

1.0 Daktari II (Medical Officer II)-Nafasi 1

1.1 SIFA

Wenye Shahada ya Udaktari kutoka vyuo vikuu vinavyotambuliwa na Serikali waliomaliza mafunzo ya kazi 'Internship' ya muda usiopungua miezi kumi na miwili na kupata usajili kutoka Baraza la Madaktari Tanganyika (Medical Council of Tanganyika)

1.2 Kazi na Majukumu

- Kufanya kazi zote za matibabu Hosipitalini zinazohusiana na magonjwa mbalimbali yakiwemo magonjwa ya Watoto, magonjwa ya kina mama na upasuaji wa kawaida wa dharura
- Kutoa na kusimamia elimu ya afya Pamoja na kuboresha afya ya jaimii katika Wilaya na Mkoa au eneo lake la kazi
- Kuchunguza, kufuatilia na kuzuia milipuko ya magonjwa
- Kutunza takwimu na kuzitumia kama ilivyoelekezwa kwenye misingi ya MTUHA.
- Kupanga na kutathimini huduma za afya katika eneo lake la kazi
- Kusimamia na kuelekeza wafanyakazi waliopo chini yake
- Kufundisha wanafunzi katika vyuo vya afya vilivyopo eneo lake la kazi
- Kubuni na kuendesha utafiti na kusambaza matokeo
- Kubuni na kutayarisha mikakati ya kuinua ubora wa huduma ya fani yake kuandaa mipango na makisio ya bajeti ya huduma za afya
- Kutoa huduma za outreach katika Wilaya/Mkoa wake
- Kufanya kazi nyingine atakazopangiwa na mkuu wake wa kazi zinazohusiana z elimu, uzoofu na ujuzi wake

MASHARTI KWA UJUMLA

- Waombaji wawe ni raia wa Tanzania
- Wawe na umri kuanzia miaka 25-35
- Waombaji waambatanishe vyeti vyote vya taaluma, Baraza sambamba na cheti cha kuzaliwa
- Waombaji waambatanishe maelezo binafsi (detailed CV) na picha ndogo (passport size) za karibuni

- Waombaji wenye uzoefu waoneshe taarifa za taasisi waliofanyia kazi Pamoja na waajiri wao
 - Awe na kitambulishi/Namba ya Utaifa kutoka NIDA
- NAMNA YA KUOMBA**

Waombaji waandike maombi yao kwa anwani ifuatayo;

MGANGA MFAWIDHI,
HOSPITALI YA RUFAA YA MT. WALBURGA NYANGAO,
S.L.P 1002,
NYANGAO, LINDI.

Pia maombi yanaweza wasilishwa kwa mkono kwa kuleta moja kwa moja au kupitia barua pepe nyangaohospital@gmail.com

Mwisho wa kupokea maombi ni tarehe **10/05/2026**

